# *ANAKUJALI*

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa tunaponena na Mwandishi wa Neno.

Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya majaliwa haya mazuri na mema ya kuja Kwako tena alasiri ya leo. Tunakuja kwa unyenyekevu katika Jina la Bwana Yesu, tukiomba msamaha wa dhambi zetu, na kwamba Wewe utatutembelea tena usiku wa leo. Na kutupa kwa wingi, sana sana kuliko yote ambayo tungeweza kufanya ama kuwazia.

2 Tunaomba kwa ajili ya kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu. Kwa wale walio wenye dhambi, kwanza, wasiokujua Wewe, kusudi usiku wa leo kuweze kuja uponyaji wa nafsi na roho yao, ili kwa jumla waweze kuwa watumishi Wako usiku wa leo. Tunaomba, Baba, ya kwamba wale ambao hawajakata kauli, kama vile tungesema, kamwe hawajui waelekee wapi, na huenda ikawa, hii iwe ndiyo nafasi yao ya mwisho. Tunaomba, Baba, ya kwamba watageuza macho yao kuelekea Mbinguni. Lijalie, Bwana.

3 Tusingewasahau wale wanaopata ahueni, walio hospitalini na nyu—nyumbani, na walio wagonjwa wala hawawezi kuhudhuria ibada, ingawa wangetaka sana, kuhudhuria. Tungeomba kwamba Malaika wa Mungu wangekaribia kando ya vitanda vyao usiku wa leo. Na labda maana tumekusanyika pamoja na kuomba, kwamba Wewe utajalia nguvu za uponyaji ziwajie, ili waweze kuja kesho usiku kwenye ibada, na kuendelea. Lijalie, Bwana.

4 Kukiwa na wengine hapa walio wagonjwa na wanaoteseka, jalia huu uwe ndio usiku wa ukombozi wao. Tubariki pamoja tunapoendelea kukungojea Wewe, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu na kwa ajili Yake. Amina.

Mwaweza kuketi.

5 Vizuri sana kurudi Nyumbani mwa Bwana usiku wa leo! Mimi, nikiingia tu mlangoni kule nje, basi nilikutana na ja—jamaa mmoja. Nilinyosha *hivi* na kuushika mkono wake, ilikuwa ni mvulana wa Ndugu John Sharrit. Sijui jinsi mvulana huyo alipata kukua sana hivyo. Nilimwuliza, kama David alikuwa mkubwa kama alivyokuwa. Na, vema, inaonekana tu kama ni mwaka mmoja uliopita, nilipokuwa hapa. Nami nafikiri imekuwa kama miaka mitatu. Lakini alikuwa tu ni mvulana mdogo akikimbia huku na huku amevaa maskini jozi ya ovaroli. Naye huyu hapa usiku wa leo, mwenye nguvu, mrefu, (vema, sidhani anasikiliza) nitasema, kijana mwanamume mwenye sura nzuri. Lakini bila shaka amekua. Na hivyo ndivyo kila kitu kinavyoenenda. Tunakulia tu mbali na sisi wenyewe.

6 Nami nilikuwa huko nje leo hii kwenye Mlima wa Camelback, ambako miaka thelathini na mitatu iliyopita niliendesha kupitia nyikani huko nje, mgongoni mwa farasi, nikawafukuza punda wadogo nyuma ya Mlima Kusini hapa. Sidhani kuna yeyote aliyesalia Arizona tena, yote imefyekewa barabara na barabara kuu. Vema, hilo hapo jambo moja, "Hapa hatuna mji udumuo; bali twautafuta Ule ujao, ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu." Ninajua ya kwamba watu wanaingia, nanyi hamna budi kutoka nje na kupanuka. Ila nilichukia tu kuona bonde la kale la mpungate likiondolewa, na kugeuzwa kuwa mradi wa ujenzi wa nyumba. Na—na inaonekana tu kama. . .Nachukia kuona hilo. Nalitumaini sitakaa muda mrefu kutosha kuona hilo. Ninii tu, na—napenda ya asili, kwa namna fulani. Loo, mna makazi mazuri, hiyo ni kweli. Lakini, hiyo—hiyo imepotoshwa, hivyo ndivyo mwanadamu amefanya. Mawazo yangu ya uzuri si kile mwanadamu amefanya, lakini mawazo yangu ya uzuri ni vile Mungu alivyoifanya. Kuangalia tu, hivyo ndivyo ninavyoipenda.

7 Lakini, taifa letu linaenda, watu wetu wanaenda, na kila kitu hapa kinaenda. Nimesimama mahali wale Mafarao wakuu waliposimama wakati mmoja, na mamlaka makuu yaliyoutawala ulimwengu, nawe ingekubidi kuchimba futi ishirini chini ya ardhi kupata magofu ya ufalme wao. Na mle ndani ambamo wale Makaisari, katika Rumi; walishuka mtaani, nao wanasema, "Futi ishirini chini ya hapa ndipo Nanii wa nanii, yule mfalme mkuu." Loo, jamani! Hapo, kwa sababu hatuna mji udumuo.

> Kwa hiyo matumaini yetu yamejengwa sio juu ya chochote
> Pungufu ya Damu ya Yesu, pamoja na haki;
> Wakati yote kando ya nafsi yangu yanapotoweka,
> Basi Yeye ndiye tumaini na nanga yangu.
>
> Juu ya Kristo Mwamba wenye imara nasimama;
> Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

Hilo ndilo tunalotazamia.

8 Na sasa, usiku wa leo, tunaona watu wamesimama pande zote. Nami nasikia kwamba kesho usiku watashuka kwenye lile jumba la mikutano, ama ninii, Madison Square Garden. Aisee, natumaini hawajalileta hilo huko magharibi sasa.

9 Kila kitu kinaelekea magharibi. Nilisikia wakati fulani uliopita, shairi dogo, lililosema, "Walibadilisha maeneo ya malishoni. . .Hapo wamashariki walipokuja magharibi, waliyabadilisha malisho yote huku nje yakawa uwanja wa gofu. Kisha wakachukua zizi la kale wakalifanya kidimbwi cha kuogelea; wakawaweka mbwa mwitu kwenye Bustani ya

New York." Kisha kasema, "Kuna kitu kimoja tu kilichosalia, hicho kilikuwa ni kamba ya kujinyonga wenyewe kwayo, juu ya mpopla." Kwa hiyo nadhani hivyo ni karibu jinsi liendavyo. Hiyo ni kweli! Naam.

10 Mliwahi kutambua ustaarabu hutoka mashariki kwenda magharibi? Na kule ustaarabu uendako, hupotosha njia yake, unapoenda. Hiyo ni kweli kabisa. Mtadhania mimi ni mtazamia mabaya usiku wa leo, sivyo? Lakini hilo . . . Ninataka kuhubiri, moja ya usiku wakati nikiwa hapa, Bwana akipenda, juu ya: hapo mashariki na magharibi zinapokutana. Na hivyo ndivyo wamefanya. Sisi . . . Ustaarabu wa kale kuliko wote ni Uchina. Na kama tukienda moja kwa moja magharibi, tunaingia moja kwa moja katika Uchina tena. Hakuna chochote ila bahari kati yetu. Nazo mashariki na magharibi hutembea pamoja.

11 Pia kumbukeni, Biblia inasema, nabii alisema kwamba, "Siku yaja ambayo haitakuwa mchana wala usiku, kidogo ni siku yenye utusitusi; lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru, katika wakati wa jioni."

12 Sasa ustaarabu umesafiri kutoka mashariki kwenda magharibi. Nalo kama jua kijiografia linavyochomoza, huchomoza mashariki na kusafiri kuelekea magharibi, nalo linatua magharibi.

13 Kwa hiyo, hebu na tuone kile M-w-a-n-a alichofanya wakati alipoileta Nuru ya Injili. Hapo mwanzo, juu ya watu wa mashariki, kulikuwako na pentekoste, umwagikaji wa Roho Mtakatifu, ishara, maajabu, miujiza, mambo makuu yakitendeka.

14 Sasa tumekuwa na siku ambayo haijakuwa usiku wala mchana, ni siku yenye utusitusi. Tumekuwa na ya kutosha ku— kujiunga na kanisa, kuandika jina letu kwenye kitabu. "Lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru." Jua lile lile linalochomoza mashariki, hutua magharibi. Na sasa Roho Mtakatifu yule mkuu, kote katika miaka, ameangaza Nuru ya kutosha kupitia katikati ya ukanisa na umadhehebu, na kadhalika, kwa ajili ya watu kuokolewa kote katika wakati.

15 Lakini Nuru za jioni zimekuja sasa! Na sasa Roho Mtakatifu yule yule, pamoja na dhihirisho lile lile, akifanya mambo yale yale, akitenda kazi tu kama alivyotenda, anaangaza juu ya watu wa magharibi, akichukua kutoka kwa Mataifa watu kwa ajili ya Jina Lake.

16 Na sasa mashariki na magharibi zimekuja pamoja, nao ustaarabu umegongana, nao umeleta moja ya hali ya dhihaka, ya kishenzi kuliko zote ambazo ulimwengu umewahi kuona ama kuota. Tutaliendea usiku mmoja; hilo silo nililokuwa nikitaka kuzungumzia usiku wa leo. Lakini hakika ni wakati, ambapo tuko kwenye wakati wa mwisho. Hilo ndilo ninalojaribu

kufanya, kuwaonya watu, daima, kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho.

17 Tufanyeje? Hakuna matumaini katika kitu chochote tena; ni katika Kristo pekee. Kumbukeni tu hilo! Kristo ndiye tegemeo la pekee tulilo nalo.

18 Hatuwezi kuiangalia demokrasia. Ilikuwa ni nzuri; bali imepita, imeishi maisha yake. Wafalme waliishi maisha yao, na falme, na watawala wa kimabavu, nao wote wamemaliza siku yao. Demokrasia ilikuwa ndicho kitu kizuri sana walichokuwa nacho. Lakini imepotoshwa sana, kupitia siasa, imeoza kabisa. Hakuna matumaini kwake hata kidogo. Ni kama tu mnajaribu kujenga kwenye mji uliochomwa moto ambao umeungua ukawa moshi. Huwezi kuujenga. Umeangamia na umeisha. Nao hauna budi kuwa hivyo. Hauna budi kuja hivyo. Biblia inasema itakuwa hivyo.

19 Shetani ndiye mtawala wa kila taifa. Kila ufalme ni wa Shetani, naye huzitawala kulingana na njia yake ya kutawala. Lakini si alizitoa kwa Mwana wa Mungu siku moja? "Hizi ni zangu, ninafanya nazo nipendavyo, falme zote za ulimwenguni." Hiyo ndiyo sababu zinapigana, na kuuana na kuangamizana kinyama.

20 Lakini Yesu alisema, "Rudi nyuma Yangu, Shetani."

21 Kwa kuwa, Yeye alijua atazirithi. "Basi furahini, enyi mbingu nanyi manabii watakatifu, kwa kuwa ufalme wa ulimwengu huu umekuwa Ufalme wa Bwana wetu, Naye atauongoza na kuutawala kwa miaka elfu moja." Ndipo hakutakuwako na vita tena. Loo, Siku hiyo kuu na ije! Loo!

22 Hebu niwashawishi, katika Jina la Kristo! Enyi watu wa thamani hapa, wekeni matumaini yenu yote Kwake, kwa kuwa, Yeye ndiye msingi wa pekee. Kwa kuwa, mtikiso unakuja. Demokrasia imetikiswa vipande-vipande. Falme zimetikiswa vipande-vipande. Mataifa yametikiswa vipande-vipande. Tuko kwenye mwisho wa mambo yote. "Lakini tunaupokea Ufalme usioweza kutikiswa; imara, usioweza kutikiswa, siku zote mkidumu katika rehema za Mungu." Loo, napenda hilo. Nina furaha sana, usiku wa leo, kuwa Mkristo! Si—si—sijui yale ningeweza kufanya kama sikuwa Mkristo. Labda ningekuwa wa kujinyonga kama sikuwa Mkristo. Kwa kuwa, nikijua na kuyaona mambo haya, halafu—halafu basi pamoja na karama ambayo Bwana amenipa, kuona kimbele na kufahamu yale Yeye ataniruhusu kufanya, kuniruhusu tu kuyaona. Ninajua ni ng'ambo tu ya upeo wa macho huko, mnaona. Kuona likija karibu jinsi lilivyo, basi linanifanya kupaza sauti kwa yote yaliyo ndani yangu. Loo, itorokeni ghadhabu ijayo!

23 Mungu, uturehemu. Baba wa Mbinguni, Ee Mungu, ninaomba. Kwa namna fulani tusaidie, Bwana. Tupe ufahamu wa kitu hiki kikuu kinachonyemelea kama nyoka, kinachovutia

jinsi kilivyo, ndege ambaye wakati mmoja amekuwa huru, akiketi kwenye mti. Lakini sasa huyo nyoka amemvutia. Naye ananyemelea, akifungua njia, hivi karibuni atakuwa kinywani mwake pamoja na meno yake ya sumu. Mungu, uturehemu. Jalia kila mmoja hapa usiku wa leo, ambaye hajatiwa nanga kikamilifu katika Kristo Yesu Mwana wa Mungu, jalia waje usiku wa leo na kuzaliwa upya kwa Roho, Bwana, kusudi matumaini yao yawe kwenye Kuja Kwake, "Wote wanaopenda Kuja Kwake." Lijalie, Bwana. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

24 Ninataka kuchukua somo langu usiku wa leo, Bwana akipenda, kutoka katika Kitabu cha Petro wa Kwanza. Na iwapo mnataka kusoma pamoja nami, Petro wa Kwanza, mlango wa 5, na hebu tuanzie kwenye kifungu cha 5. Petro wa Kwanza 5, kuanzia 5.

> *Vivyo hivyo* ninyi *vijana, watiini* wazee. *Naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana: kwa sababu Mungu* huwapinga *wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema.*
>
> *Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa* majira *yake:*
>
> *Huku mkimtwika yeye* fadhaa *zenu zote; kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.*

25 Ni somo zuri jinsi gani la Maandiko! Sasa, ningetaka kuchukua hili kwa ajili ya somo: *Anakujali.*

26 Na pia imeandikwa, katika mlango wa 14 wa Yohana Mtakatifu.

> *Msifadhaike* mioyoni *mwenu:* kama mlimwamini *Mungu, niaminini na mimi.*
>
> Kwa kuwa *nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi:* isingalikuwa *hivyo ningaliwaambia.* Nitaenda *kuwaandalia mahali.*
>
> *Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali,* nitarudi *tena, nikawakaribishe kwangu*; *ili nilipo mimi, nanyi mwepo.*

27 Tamshi lingine la Maandiko, ni kwamba Yeye atamwomba Baba, Naye angetupa "Mfariji mwingine." "Naye Mfariji huyo angekuwa ni Roho Mtakatifu, ambaye ulimwengu haungeweza kumpokea, bali angekuwa ni Mfariji kwa mwaminio. Basi atakapokuja, Yeye atanishuhudia Mimi, na kuwakumbusha mambo, ambayo nimewafundisha, na atawaonyesha mambo yajayo. Roho Mtakatifu mbarikiwa!"

28 Na katika siku za Paulo, wakati yeye aliposema: "Kama sisi. . .mtu asiyefunzwa akija miongoni mwenu, nanyi nyote mseme kwa lugha, na kusiwe na mfasiri, basi asiyeamini atasema ninyi ni wendawazimu. Lakini kukiweko na mmoja anayetoa

unabii na kufunua siri za moyo," kasema, "basi wataanguka chini na kusema hakika Mungu yu pamoja nanyi."

29 Basi sisi hapa katika siku hii, pamoja na Mfariji yuyo huyo akijidhihirisha Mwenyewe vile vile alivyofanya wakati huo. Ni faraja jinsi gani, pamoja na ahadi!

30 Sasa, kila mtu hana Mfariji huyu wa ajabu. Ha—ha—hawana. Wanamkataa, wanamkataa kwa sababu kamwe hawamwamini.

31 Kunayo njia moja tu ambayo kamwe utaweza kumpokea Mfariji huyu wa ajabu, ni utakapomwamini Bwana Yesu Kristo; ukiri dhambi zako, utubu, uhudumiwe ubatizo wa Kikristo, na ahadi kwamba Mungu atakujaza na Roho Mtakatifu. Hiyo ni ahadi Yake. Hawezi kuighairi Hiyo. Ni ahadi Yake. Nimesema sikuzote, kama mtu alifunzwa vizuri sana; naye alitubu na, kutoka moyoni mwao, alikuwa amemwamini Mungu kwa yote yaliyokuwa ndani yao; ndipo hapo wanapobatizwa, mara Roho Mtakatifu atakuja juu yao, kwa sababu Yeye aliahidi kufanya hivyo. Aliliahidi. "Mtampokea Roho Mtakatifu, kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu!"

32 Sasa, watu siku hizi, sababu ya wao kutompokea Huyo, ni kwa sababu anaingilia maisha yao ya kiroho wanayopenda kuishi. Biblia ilisema ya kwamba, "Ulimwengu, watu, walipenda giza kuliko Nuru, kwa sababu matendo yao ni maovu." Na mtu anayependa kutembea gizani na kufanya mambo maovu, ni . . . anayependa mambo maovu, hawezi kumpenda Roho Mtakatifu. Kwa sababu, Biblia ilisema, "Ukiipenda dunia, au mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako."

33 Sasa, huenda mliyasikia Maandiko haya hapo awali, bali na tuyatii. Je, Hayo ni kweli? Hayo ni ya kweli zaidi kuliko vile mmeketi humu kanisani usiku wa leo. Hayo ni ya kweli zaidi kuliko kuwa huu ni mkoa wa Arizona. Ni ya kweli zaidi kuliko wewe ulivyo mwanadamu aliye hai. Hayo ni Maneno ya Milele ya Mungu, na ahadi Zake. Na mbingu zote na nchi zitapita, bali hayo Maneno hayatapita kamwe. Yana maana; maana, adhimu. Bali kamwe hayatamaanisha kitu kwako mpaka Mungu akufunulie. Ni vizuri jinsi gani kujua ya kwamba Yeye hutushughulikia! Kwa hiyo iwapo . . .

34 Mwanadamu, aliumbwa apate kuwa na shauku ya kufarijiwa. Kwa hiyo basi asipoikubali njia ya Mungu, basi atajichukulia njia yake mwenyewe. Naye atajaribu kuweka kitu fulani kupachukua mahali pa huyo Roho Mtakatifu. Loo, ninawatakeni mlisikilize! Mwanamume ama mwanamke, ambaye hatamkubali Roho Mtakatifu, Mfariji, watajaribu kujifariji wenyewe kwa kibadala katili ambacho Shetani atawakabidhi. Shetani ana vibadala vingi sana. Lakini ni kwa nini tuwe na kibadala, wakati anga za kipentekoste zimejaa kilicho halisi? Kwa nini nile kutoka kwenye pipa la takataka wakati meza safi imewekwa imejaa chakula kizuri sana?

Ningekuwa na kasoro kiakili kama ningalifanya hivyo. Sasa, ni huzuni jinsi gani kuona kwamba mwanadamu atajaribu kuweka kibadala fulani kupachukua mahali Hapo. Wakati mwingine atajaribu kutuliza dhamira yake kwa kutoka nje. . .

35 Kama vile mama wakati mwingine atajaribu kuwafundisha wasichana wao wadogo kuwa maarufu. Kuwafanya. . .Wao, shauku yao yote ni kumfanya msichana huyo m—mchezaji rumba ama kitu fulani. Nawe unajua ya kwamba unampa sumu kali ya kusisimua neva, unampa aseniki ambayo haitafanya kitu ila kuuvunja moyo wake na kumtupa kwenye kaburi la ibilisi, ama kuzimu kwa ibilisi na kaburi la mwenye dhambi, kwa kuwa hakuna chochote chema kinachoweza kutoka kwake. Lakini unajaribu kuwazia, "Laiti binti yangu angeweza kuwa hivi na vile!" Nanyi mtawatuma hata huko kwa YWCA zetu, ambako wanacheza roki. Nao wazee watatoka nje wakacheze dansi ya vibandani, ama namna fulani ya dansi ya karamu.

36 Wanapofikia umri wa yapata miaka thelathini, wanashikwa na fadhaa. Wanawazia kwamba, "Basi kwa kuwa nimekuwa mzee hivi, sijaponda raha ya ujanani vya kutosha bado." Nao—nao wakati mwingine wanajaribu kudanganya katika nadhiri zao za ndoa, wanaume na wanawake pia. Wote wawili wana hatia! Kuna shida gani? Ni kitu fulani walichopungukiwa nacho.

37 Wakati mwingine wanaanza kunywa pombe. Ndipo wakiisha kupata umri mkubwa zaidi, mbona, watashuka kwenye chumba cha pombe, nao wataanza kunywa. Basi, wakinywa, na kujaribu kuisahau kwa kunywa pombe. Vinywaji vichache tu, na—na kisha kinasababisha vinywaji zaidi, ndipo baada ya kitambo kidogo wanakuwa walevi sugu.

38 Na wakati mwingine wapate kuwa maarufu, wataangalia televisheni kwenye. . .na mitaani, na kuvuta sigara. Jambo duni sana ambalo wanawake wamefanya katika karne ya ishirini, ni hapo wanawake walipoanza kuvuta sigara. Hao ndio vibaraka wasaliti wakuu sana taifa hili lililopata kuwa nao. Huvunja uadilifu, hu—hu—hujaza hospitali hizi huku nje na wendawazimu, inajaza hospitali kwa wagonjwa wa kifua kikuu, kansa. Na kila kitu kikitokana na hayo, na hata hivyo wanafanya hivyo wapate faraja!

39 Mungu alitupatia kitu cha kutufariji, Roho Mtakatifu, Mfariji wa Mungu! Mambo haya ni kibadala tu ambacho hatimaye kitaelekeza kwenye mahali pa matatizo chungu nzima, na udanganyifu, na wizi, na kufanya mambo mabaya.

40 Msichana wangu mdogo aliniuliza hivi majuzi usiku, akasema. . .Ama, ilikuwa ni mtoto Joseph, akasema, "Baba, kuna kitu kama mchawi?"

Nikasema, "Loo, hakika."

41 Akasema, "Je, ana pua ndefu, naye anaendesha ufagio usiku?"

42 Nikasema, "La. Yuna uso uliopodolewa, naye huendesha Kadilaki kwenda kwenye ka—karamu ya kokteli." Hilo ndilo toleo lake jipya la kisasa.

43 Naye akasema, "Huyo ni mchawi?" Sijui kama nilipaswa kumwambia hivyo ama la, kwa sababu kila wakati mtaani anapomwona mmoja, yeye husema, "Baba, yule pale mchawi. Sivyo?" Vema, nadhani kwamba . . .

44 Mnajua, walizoea kuwa na maskini Charlie Barleycorn. Baadhi yenu watu wa zamani kidogo mnamkumbuka, amevaa kofia iliyovutwa juu ya masikio yake. Na hata kunguru angemwogopa, Charlie Barleycorn. Loo, amebadilika tangu pombe ilipopigwa marufuku. Lakini sasa yeye yuko kwenye kitu kidogo, kilichopachikwa katika kila sanduku la barafu, naye ndiye jamaa maarufu sana mjini. Lakini angali ni kitu kile kile kilicholaaniwa kinachoipeleka nafsi ya mtu kuzimuni, na vijana kwenye hospitali ya wendawazimu; nao wana rika hapa juu ya mabaradhuli wa roki na wapinga maadili, na uhalifu wa vijana hata imekuwa ni wendawazimu. Hata mpaka shule zetu haziwezi kuwagusa; tulipoteza waalimu elfu ishirini mwaka uliopita.

45 Kwa nini? Wanatafuta kitu Fulani. Wanakitafuta, nalo kanisa limeshindwa kuwapa. Sababu ya wao kufanya hivyo, ni kwa sababu waliumbwa hivyo, wapate kutafuta.

46 Hatimaye, inaishia wapi? Mauaji na kujinyonga. Mwanamume anayefikiria ya kwamba anafanya jambo fulani anapopata miadi na mke wa jirani yake, ama angeivunja nyumba fulani ama mwanamke fulani. Unafikiri unapita na kitu fulani, lakini hatimaye utaishia kwa bastola upande mmoja wa kichwa chako, na kulipuliwa ubongo wako, ama kuruka kutoka jukwaani mahali fulani, ama kujiua, kunywa sumu, kasumba, ama chochote kile, na kuingia katika hali ya mashaka, kisha ufe na kwenda kwenye kuzimu ya shetani, kwa sababu umeikataa ile—ile Tiba halisi.

47 Tunayo tiba. Kalvari ndiyo tiba hiyo. Kristo ndiye hiyo tiba. Naye Ndiye tiba ya pekee, msingi wa pekee, njia ya pekee. Kuna vitu unavyoweza kupata kwa Kristo ambavyo huwezi kupata kutoka mahali pengine. Kristo ndiye njia; sio njia *fulani*, Yeye ndiye *ile* njia. Kanisa ni sawa, tunayapenda, bali kanisa silo njia. Yesu ndiye njia! Huwezi kulitwika kanisa fadhaa zako, kanisa halina wokovu. Linaweza tu kukuelekeza kwa Yesu, Ambaye ndiye wokovu pekee. Yeye ndiye Njia, Kweli, Uzima. Njia pekee ya kwenda kwa Baba ni kupitia kwa Yesu! Mfariji pekee, Yule pekee awezaye, anayejua jinsi ya kutushughulikia.

48 Kwa kuwa, hata hatuwezi kushughulikiana sisi kwa sisi. Nilisoma katika Maandiko wakati fulani uliopita, ambapo yalisema, "Kutokuupambanua Mwili wa Bwana." Nami

nikawazia, ni tamshi la jinsi gani! Linapatikana katika Wakorintho wa Kwanza 11.

> . . .*kwa kutokuupambanua mwili wa Bwana.*
>
> Na *kwa sababu hii wengi ni* wagonjwa *na* dhaifu *miongoni mwenu* . . .

49 Mwili wa Bwana ni Kanisa. Nasi hatuna upambanuzi wa kiroho wa kutosha kujaliana. Tunawezaje kujali basi iwapo hatuwezi kujaliana? Tunawezaje kuwajali waliopotea na wanaokufa? Ni hospitali gani tunayoweza kuwapeleka? "Tumtwike fadhaa zetu, kwa kuwa Yeye anakujali."

50 Wanaume huchukua njia hizi za mkato, na kinachowafanya wafanye hivyo ni kwa sababu . . . Mungu, alipomwumba mwanadamu, Yeye hakumwumba mwanadamu apate kufanya hivyo. Alimwumba mwanadamu awe mwenye furaha, kuridhika, na kufarijika. Mwanadamu . . . Mungu hawataki watoto wake kukosa faraja. Usingeninii . . .

51 Mbona, ninyi akina mama mngeamka kati kati ya usiku, kama mlikuwa wagonjwa sana; kama kadogo alikuwa ameondolewa blanketi, nawe unajua maskini jamaa huyo mdogo angeshikwa na homa, ungejitahidi kwa njia fulani upate kwenda kando ya hicho kitanda, ukamfanye kustarehe. Kama mmoja wa wapendwa wako alikuwa ameshikwa na homa, nawe ungeweza kukaa pale na kitambaa na kuosha uso wao kwa maji baridi, kuwastarehesha; ungefanya hivyo, mmoja wa watoto wako. Ungeketi pale, ingawa ulikuwa mgonjwa na ulipaswa kuwa kitandani wewe mwenyewe, bado ungeketi pale, kwa maana watoto wako wanamaanisha kitu kwako. Wao ni sehemu yako, wao ni maisha yako.

52 Nalo Kanisa ni Maisha ya Mungu, duniani, Naye anataka kulistarehesha Kanisa Lake.

53 Na jinsi ingekuwa, kama ulijua ya kwamba kuupangusa uso wenye homa wa mtoto wako kungemtuliza. Naye angekataa, na kukutemea mate usoni mwako, na kuchukua chupa ya wiski ama kitu fulani anywe, badala, badala ya ule mguso wa mkono wa mama ama chochote kile.

54 Hivyo ndivyo tunavyofanya tunapoziendea tiba zingine. Kuna dawa nyingi, bali Tiba moja. Kristo ndiye hiyo tiba, na tiba pekee katika jambo hili. Yeye anatujali. Anatupenda, Naye anatutaka tumjie. Mungu alituumba jinsi hiyo, kitu hicho kitakatifu ndani yetu kinachotaka kufarijiwa.

55 Mungu alimpa mwanamume mke, apate kumfariji, kumgusa. Na mwanamume yeyote anajua, aliye na mke mzuri, kuna jambo fulani kuhusu mke mzuri anayeweza . . . Mwanamume anaweza kufadhaishwa katika biashara yake ama—ama shughuli yake, naye anaweza kuja nyumbani; haijalishi, hakuna mtu, hakuna daktari . . .

56 Ndivyo ilivyo kwangu mimi. Ninaporudi kutoka nchi za ng'ambo ama mahali fulani, nami nina wasiwasi sana na nimefadhaika, na kupoteza usingizi. Na—na kusikia kilio, na kuona maskini watoto wadogo wenye njaa mtaani, na, loo, wakilia na kuendelea, linaniua tu. Ndipo ninapokuja nyumbani, kama mke ataketi juu ya mkono wa kiti, anikumbatie kwa mkono wake, na kusema, "Loo, Bill, na—naelewa hilo, wajua."

57 Basi mipapaso michache tu kutoka kwa mke inamaanisha mengi sana; jambo lile lile, mume kwa mke. Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka iwe. Basi tunapoweka kitu fulani badala ya hilo, nawe utamchukua mwanamke mwingine kujaribu kupachukua mahali hapo, ama mwanamume mwingine, unaona kile unachofanya.

58 Sasa, mbona, Yeye alitupa marafiki. Anapenda. . . Sisi, sisi tunapaswa kuwa marafiki. Tunapaswa kuwa ndugu. Na jinsi ambavyo ni vizuri kumwendea rafiki mzuri, katika wakati wa shida, na kusema, "Loo, ewe rafiki yangu, mambo fulani na fulani yametukia." Naye rafiki mzuri, anayeaminika aketi chini na kuzungumza nawe, hilo ni zuri sana. Huyo ni wa Mungu. Kama tu vile mke wako alivyo wa Mungu, mume wako, unapokuwa mwaminifu.

59 Lakini imefikia ambapo hata katika mwanadamu, kuonyesha asili yake iliyoanguka, yeye hudhalilisha kile ambacho Mungu amempa. Jambo la kwanza, yeye alichukua chupa, ama ulimwengu, kumfariji badala ya Roho Mtakatifu. Mungu alimpa mke apate kuwa mwenziwe wa maisha, wala yeye haridhishwi na mmoja, inambidi kumchukua mwingine na mwingine; mwanamke kwa mwanamume, au kinyume chake. Vijana, na kadhalika.

60 Na hata hao wafariji wote ambao Bwana ametupatia! Inapofikia mwisho wa safari, nasi tunasukuma foronya kwenye uso wetu wenye homa, na kufa. Mke wetu anaweza tu kusimama, na machozi yakitiririka usoni mwake, huku amemwinulia Mungu macho yake. Rafiki yetu anaweza kutupigapiga begani na kutupa mikono; na kusimama, akiiminya mikono yake, kwa sababu hawezi kwenda mbele zaidi. Lakini basi wakati Mfariji, kama Daudi alivyosema, "Naam, nijapotembea kwenye bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya. Wewe upo pamoja nami. Gongo Lako na fimbo Yako vyanifariji, hata katika bonde la vivuli vya mauti."

61 Ni kwa nini watu huona kiu na kuona njaa? Kwa sababu, wakati alipoumbwa, alifanywa na kuumbwa akiwa na mahali padogo ndani yake ambamo Mungu aliishi, kumfariji. Basi alipojiondoa kwa Mungu, kwa dhambi, basi mahali hapo pakawa patupu. Na hiyo ndiyo sababu anamwonea njaa, anamtafuta.

62 Nayo shida siku hizi, kwetu sisi Wakristo, nahofia hatufanyi yote tuwezayo kufanya kumwonyesha ndugu yetu aliyeanguka ya kwamba hiyo ndiyo shida yake. Hiyo ndiyo shida ya uhalifu wa vijana, ni kwa sababu kumekuwako na uhalifu kanisani na uhalifu nyumbani, ambao umesababisha uhalifu wa vijana.

63 Hiyo ndiyo sababu wapinga maadili na kadhalika wako mitaani, wakiruka-ruka, na kuyakuza mambo haya yote, ni kwa sababu wanajaribu kupata kitu cha kuridhisha.

64 Hebu niseme jambo hili usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu! Hakuna kitu kitakachoridhisha kama kule kuja kwa Nguvu za Roho Mtakatifu, ambazo zitayabadilisha maisha na misimamo yako, na kukupa faraja na Uzima wa Milele.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Wenye dhambi wanapotumbukizwa chini ya hilo gharika,
Hupoteza waa lao lote la dhambi.

65 Mke anaweza kufariji na kupigapiga. Rafiki anaweza kuketi chini na kutoa mawaidha mazuri. Lakini kuna Kitu kimoja tu kinachoweza kuondoa dhambi, hicho ni Damu ya Bwana Yesu!

Ni kitu gani kinachoweza kuziondolea dhambi zangu?
Hakuna chochote ila Damu yake Yesu;
Ni nini kinachoweza kunifanya mzima tena?
Hakuna chochote ila Damu yake Yesu.

Kama huyo mwandishi alivyosema:

Loo, mtiririko huo ni wa thamani
Unaonifanya mweupe kama theluji;
Sijui chemchemi nyingine,
Hakuna chochote ila Damu yake Yesu.

66 Jambo ndilo hilo! Hiyo husafisha na kutakasa, na kuingiza katika ushirika. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Hata hivyo nyinyi mtaniona, kwa kuwa Mimi" (kiwakilishi nafsi) "nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Naye Huyo Roho Mtakatifu atakapokuja, Yeye atakuja, awe Mfariji atakayetumwa na Baba katika Jina Langu. Yeye atawaonyesha mambo yajayo, na kuwakumbusha mambo." Lini? Tunapoketi pamoja mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, Roho Mtakatifu akija kupitia kwenye Neno, akishuka, akifariji, akitoa faraja.

67 Kule kuja kwa maangamizi ya ulimwengu! Mambo yote ambayo yamekuwako sasa yanatoweka. Matumaini yote yametoweka, wala ulimwengu hauna mahali popote pa kusimama. Wanakunywa, wanacheza karata, wanaoa, wanaolewa, kwa sababu wamekataa ule Msingi wa kweli wa faraja, Roho Mtakatifu.

68 Lakini sisi tunaomwamini Yeye, tunautazamia Ufalme ujao (Jina la Bwana na libarikiwe!), ambako hakutakuwako na huzuni tena, wala kulia, wala huzuni kubwa; bali amani, na furaha, na upendo, na kutopatikana na mauti, vitachukua mahali pake siku moja.

69 Mtwikeni fadhaa zenu! Endapo mna shida, mtwikeni Yeye, kwa kuwa Yeye anawajali. Hiyo nyingine inaelekeza kwenye mauti ya Milele. Hii inaelekeza kwenye Uzima wa Milele. Naye mwanadamu ameumbwa hivi kwamba angemhitaji Mfariji huyo. Anamtaka mfariji, kwa sababu aliumbwa hivyo. Hivyo ndivyo Mungu alivyomweka pamoja, akavijenga hivyo vyumba ndani yake; nafsi yake, dhamira yake, macho yake, hisia zake, kila kitu kiliwekwa pamoja. Na katika chumba hiki kidogo, cha kitu fulani cha kumfurahisha, kumpa faraja, kuondoa uchovu na wasiwasi kutoka kwake, Mungu aliketi pale pamoja na Roho Mtakatifu. Loo, ni picha ya jinsi gani! Ni ukweli jinsi gani!

70 Sasa, maskini rafiki yangu mwenye huzuni nyingi, endapo upo hapa wala hujui hilo, mimi ni shahidi kwamba hiyo ni kweli. Mimi ni mtu mwenye wasiwasi, mwenye huzuni. Mwairishi, pande zote mbili, na—nao wana wasiwasi na ni walevi. Naye mama yangu ni nusu Mhindi. Ambalo, kwa kweli, kwa kuzaliwa, lingenifanya mwasi. Hiyo ni kweli. Loo, ningekuwa mtu mbaya sana, chotara, karibu hivyo. Lakini ni kitu gani kilichotukia? Nilipata kitu kilichokichukua chumba hicho kidogo ndani yangu, na kunipa amani ipitayo ufahamu, nami nimetoka mautini kuingia Uzimani, kutoka gizani kuingia Nuruni. Loo, kamwe nisingeweza kumkana Huyo. Huyo ndiye Uzima wangu. Yeye ni yote!

71 Nikisimama huko hospitalini, nilipokaribia kabisa miaka thelathini na mitatu ya huduma yangu, nusura nijisalimishe kwa Shetani. Wakati maskini msichana wangu mdogo, Sharon Rose, alipokuwa akifa hospitalini. Nami nikasimama pale, wala daktari hata hakujua nilikuwa chumbani.

72 Asingeniruhusu kuingia, kwa sababu alikuwa na homa ya uti wa mgongo. Akasema, “Billy, utamwambukiza Billy Mdogo. Usiingie mle.”

Nami nikasema, “Doc!” Ndipo akaniketisha chini.

73 Akamwambia nesi, kasema, “Nenda kalete dawa, umpe.”

74 Akatokea na glasi ndogo, ndefu *hivi*, akasema, “Kunywa hii, Ndugu Branham.”

75 Nami nikasema, “Iweke tu chini.” Nami nikamwangalia mpaka akatoka chumbani. Nami huyo nikashuka sebuleni, na kuingia kwenye chumba cha chini!

76 Naye huyo hapo mtoto wangu amelala, amelala pale huku nzi wakiwa machoni mwake. Maskini ukanda mdogo wa mbu umewekwa juu ya uso wake, akautupilia mbali.

Ndipo nikamwangalia mama wa jamaa huyo mdogo amelala pale kwenye nyumba ya maiti. Maskini ndugu yake, Billy, hospitalini, mahututi. Baba yangu alikuwa tu amefia mikononi mwangu, majuma machache hapo kabla. Naye ndugu yangu akauawa, kwa ghafla. Mambo ndiyo hayo, nami si kitu ila mvulana mhubiri! Nikamwangalia, nami nikaangalia. Nikasema, "Loo, Sharon, kipenzi! Huyu ni baba, unanijua mimi?" Nami ninajua alinifahamu. Alikuwa akijaribu, ilivyoonekana, kuniaga kwa kupunga mkono. Nayo macho yake madogo yalikuwa yakiingia makengeza. Alikuwa anaumwa vikali, nikayaona maskini macho hayo ya bluu yakiingia makengeza.

77 Ndipo basi nikamwangalia. Nami nikapiga magoti, na kusema, "Mungu, mama yake amelala huko katika—katika nyumba ya maiti, tutamzika asubuhi. Usimchukue mtoto wangu mchanga, Bwana. Jalia nimlee. Yeye ni mzuri sana! Wala usimchukue, Bwana." Mara, ilionekana kama shuka jeusi lilitokea, likikunjuliwa, likalifunika tu hilo ono kutoka kwake. "Unamchukua, kwa vyovyote vile!" Nikasimama.

78 Ndipo basi Shetani akaja karibu nami, na kusema, "Halafu ati ungemtumikia? Wewe huyu hapa, si kitu ila mvulana. Nawe unamaanisha . . . Umefanya nini? Umesimama kando ya barabara kila mahali ulipoweza, na kufunga mpaka ukawa dhaifu sana usingeweza kupanda nguzo ya simu, kufanya kazi yako. Nawe umefanya nini ila kuhubiri na kulia na kuomba? Na neno moja kutoka Kwake lingebadilisha picha yote, lakini je, Yeye angefanya hilo? La, hatalifanya. Atamwacha afe. Halafu ati utageuka na kumtumikia?" Nilikaribia sana, katika saa hiyo . . .

79 Wakati miguu yangu isingenishikilia tena, niliegemea kitandani. Nikasema, "Sharry, unamjua baba." Naye angeninii . . . kumsikia kama anakorota, naye angeangalia. Na—najua alikuwa yuafa.

80 Nikawazia, "Neno moja tu! Isingembidi hata kulinena, ni kuangalia tu; nia Yake mwenyewe ingeliibadilisha tu picha hiyo, nayo hiyo homa ya uti wa mgongo ingemwacha naye angepona. Neno moja tu! Lakini hata hivyo Yeye asingefanya hivyo."

Shetani akasema, "Halafu utaendelea tu kumtumikia?"

81 Nami nikawazia, "Niende wapi? Ningefanya nini? Ningeenda kwa nani? Liko wapi tumaini langu? Jambo fulani likatukia kwangu," nikasema, "miaka michache iliyopita hapa chini, nami najua ya kwamba nampenda!"

82 Nikajongea kwenye kitanda, nikaweka mkono wangu juu ya kichwa chake kidogo, nikasema, "Kipenzi, Mungu alikuleta, na Mungu anakuchukua, Jina la Bwana libarikiwe!"

"Hata ukiniua, hata hivyo nitakutumaini!" Naam, bwana!

83 Nikasema, “Nitakuchukua, kipenzi, na kukulaza juu ya mkono wa mama yako huko kwenye—kwenye nyumba ya maiti ya mtayarisha mazishi, katika yapata saa moja kuanzia sasa. Lakini hata hivyo kama Yeye akiniua, hakuna kitu ninachoweza kukiendea. Yeye ndiye tumaini la pekee nililowahi kuona. Yeye ndiye msingi pekee. Yeye ndiye faraja pekee niliyowahi kuwa nayo. Basi ningeweza kwenda wapi sasa kupata faraja, kama haikuwa ni Kwake?”

84 Niliposema hivyo, Malaika walikuja wakamchukua. Nami karibu tu nizimie, bali jambo fulani likatukia! Yeye alikuwa ndiye Mfariji wangu. Alinijia. Akanishughulikia.

85 Nikaenda hadi kaburini, siku baada ya siku, kutimiza wajibu wa kwenda huko kila siku, kuomboleza kidogo na kuomba. Mbunge wa mkoa alikuwa ni mshiriki wa kanisa langu, kanisa la Kibaptisti. Na kwa hiyo basi ni—nilikuwa ninaenda zangu barabarani, ndipo Bw. Isler, yeye akasema . . . Akakaribia na kuniona, akasimama, ndipo akakimbia hapo na kunikumbatia kwa mikono yake. Nilikuwa nimevaa buti, ilikuwa ni mara baada ya yale mafuriko ya mwaka wa ’37. Basi nilikuwa nikienda zangu barabarani, mikono yangu nyuma yangu. Naye Bw. Isler akasimama, akanikimbilia, akasema, “Billy, ninataka kukuuliza jambo fulani, mwanangu.” Yeye ni mzee, angali anaishi, kwenye miaka yake ya mwishoni kabisa sasa.

Nami nikasema, “Ni kitu gani, Bw. Isler?”

86 Akasema, “Nimekusikia ukihubiri. Nimekusikia ukizungumza, na jinsi ulivyomtukuza Kristo na kusema mambo haya yote kumhusu Yeye! Naye hapo akamwacha baba yako afie mkononi mwako, kwa kuzidishiwa dawa ambako kulimwua.”

87 Daktari alimwua. Pasipo kujua alichokuwa akifanya, alimpa nusu chembe ya sumu kali ya kusisimua neva, nayo ikamwua. Nami . . . Basi akafa papo hapo mikononi mwangu, akinitazama usoni.

88 Siku mbili ama tatu baada ya hapo, nilimtazama Mkristo mpendwa, shemeji yangu, mke wa ndugu yangu, akifa; nikamwona akisimama na kumwangalia robini aliyeketi mtini, na kuimba, “Kuna Nchi ng’ambo ya mto.”

89 Hapo mke wangu alikufa, nikimshika mkono, akisema, “Bill, umezugumza juu yake, umehubiri juu yake, bali hujui jinsi ilivyo tukufu kuondoka kwenye maisha haya hadi Mengine.” Mambo hayo yote kule niliyokuwa nimemwona Yeye akiyafanya!

90 Na, loo, yeye alisema, “Sasa Yeye amechukua kila kitu ulicho nacho, Yeye anamaanisha nini kwako sasa?”

91 Nikasema, "'Wewe kijito cha faraja yangu yote, zaidi, ya maisha kwangu; ni nani niliye naye duniani mbali na Wewe, ama ni nani Mbinguni ila Wewe?' Loo!"

Akasema, "Inamaanisha hivyo kwako?" Nikasema, "Inamaanisha hivyo kwangu!"

92 Nikasonga mbele nikaenda upande mmoja wa kilima pale ambapo alizikwa. Ndipo nikaketi pale muda kidogo, na ilionekana kana kwamba maskini hua mmoja alitokea, angeimba, ama angelia, jioni kabisa wakati nimeketi pale na kumwazia mke, na mtoto aliyelala hapo chini mkononi mwake, basi ilionekana kana kwamba upepo mwanana ukipulizia kwenye misonabari, ungeimba:

Kuna Nchi ng'ambo ya mto,
Wanaiita tamu milele,
Na tunaifikia tu pwani hiyo kwa mkataa wa
imani;
Mmoja baada ya mwingine twaingia langoni,
Huko tukaishi pamoja na wasiopatikana na
mauti,
Siku moja watapiga hizo kengele za dhahabu
kwa ajili yako na yangu.

93 Mambo ya mwisho niliyomwambia mke wangu wakati alipokufa, nami nikamuaga kwa busu. Akasema, "Usiishi bila mwenzi, Billy. Mchukue mwanamke mzuri aliyejazwa na Roho wa Mungu, akawalee watoto wangu." Hakujua huyo mtoto mchanga alikuwa anaenda kufa kesho yake. Naye akasema, "Nitakutana nawe asubuhi ile." Akasema . . .

94 Nikasema, "Simama kule upande wa mashariki mwa lile lango. Ndipo utakapomwona Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, na hao watoto wa Ufalme wakiingia, anza tu kupiga makelele, 'Bill! Bill! kwa sauti uwezavyo. Nitawakusanya watoto pamoja na kukulaki pale." Hiyo ilikuwa ndiyo miadi yangu ya mwisho naye. Na kwa msaada wa Mungu, ningali nitamtwika fadhaa zangu zote, pamoja na faraja ya Roho Mtakatifu, ili siku moja nitimize miadi hiyo, nitakapokutana naye kule.

95 Kwa neema ya Mungu, nitadumu kwenye uwanja wa vita na kuhubiri mpaka maisha yangu yaishie kwenye Ufalme wa Mungu.

96 Loo, mtwikeni fadhaa zenu, Yeye anawajali. Sasa Yeye anawajali, sasa tunajua. Hebu tuulize, dakika chache, kama Yeye anatujali. Vema.

97 Yeye alimshughulikia yule mwenye ukoma wakati alipokuwa hapa duniani. Huyo hapo mwenye ukoma ameketi.

98 Mlipata kumwona mwenye ukoma? Loo, nimeona wengi wao, nikawakumbatia mikononi mwangu, hao wakiwa weupe kwa

ukoma. Wanaonekana kama dutu la mbegu lililogeuzwa ndani nje.

99 Ameketi ambapo hapana mtu angemgusa, huko chini kwenye vinamasi na uchafu na kinyaa cha mtaani, duni alivyoweza kuwa, ambapo kila mtu aliogopa kumkaribia. Yeye alikuwa. . . Alikuwa mtu aliyetengwa na jamii. Alitengwa na jamii ya mji, na jamii ya kanisa na jamii ya—ya kila kitu kilichokuwako mjini. Hakuna mtu aliyetaka uhusiano wowote naye. Kama walifanya chochote, wangemtupia kipande cha mkate na kumwacha akiokote huko mavumbini. Wasingemkaribia.

100 Lakini Yesu alijishughulisha naye. Alitembea moja kwa moja pamoja naye, kisha akaketi. Ninaweza tu kumwona akiweka mikono Yake juu yake, na kusema, "Nataka, na utakasike." Loo, alimshughulikia. Wakati hakuna kingine kingemshughulikia, Yeye alijali.

101 Wakati hakuna kingine kitakachokujali, Yeye angali anajali!

102 Palikuwako na maskini mwombaji kipofu, huku mikono ya shati lake imeraruka, masharubu kote usoni mwake, wala hana chakula, aliketi karibu na lango siku moja, akiombaomba. Naye Mwana wa Mungu, akienda Zake Kalvari, kusulubiwa, amejitwika dhambi za ulimwengu; lakini mmoja alipiga mayowe, "Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!"

103 Je, mtu mwenye hadhi hiyo, mtu, Rais, meya, gavana wa jimbo, aliye kwenye kikosi cha polisi, angeweza kusimama kwa ajili ya kitu kama hicho? Utaipata kwa nadra.

104 Lakini Yesu alijali. Alimtwika fadhaa zake, Naye akamshughulikia. Akasema, "Wataka nikufanyie nini?"

Kasema, "Bwana, nataka nipate kuona."

Yeye akasema, "Imani yako imekuokoa." Alimjali.

105 Palikuwapo na mwanamke mtovu wa maadili wakati mmoja, kama vile mlevi sugu ama kahaba, mtovu wa uadilifu sana mpaka wanawake wa mjini wasingeweza kumgusa. Alitengwa na jamii. Alitoka kwenda kuteka maji yake, ilimbidi angoje mpaka wakati wa adhuhuri. Asingeweza kuambatana na wanawake wenye sifa nzuri. Hakuna mtu angalitaka uhusiano wowote na huyo mwanamke. Alikuwa ameolewa, naye alikuwa na lundo la waume, naye ni kimada wakati huo. Hakuna mtu aliyemjali. Walikuwa wagumu sana na baridi. Hakuna aliyejali!

106 Lakini Yeye alimjali sana hata akamwambia siri za moyo wake, kisha akamsamehe kila dhambi. Kisha akaweka kitu Fulani ndani yake, hata akakimbia mjini, akisema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyoyatenda."

107 Mnaona, hilo ndilo linalomfanya Yeye mkuu kwangu. Yeye hana majivuno. Alikuwa ni neema ya Mungu kwa watu. Alikuwa ni upendo wa Mungu uliodhihirishwa katika mwili wa

mwanadamu. Haidhuru ni mdogo jinsi gani ama asiye na faida, Yeye aliwajali; watovu wa uadilifu, walevi, walevi sugu, wowote wale.

108 Ninamwazia maskini Rosella Griffith, huko Chicago. Kitabu chake kitatolewa sasa. Huyo alikuja mkutanoni, mpotovu sana hata lile—lile Shirika kuu la Walevi Sugu lilikuwa limemkataa. Na yapata hospitali sita ama nane maarufu za Chicago zilikuwa zimelifuta jina lake kwenye kitabu, "kamwe asiende" kule. Mpaka hata alikuwa duni sana, mpaka kitu pekee alichokuwa nacho kilikuwa ni koti ambalo mama yake alimpa; akalikata upande wa ndani na kuweka chupa zake mle ndani, mlevi sugu kweli kweli, asije akaganda hata kufa, akilala kwenye mitaro usiku. Msichana, mwerevu, mwenye elimu; mwanamke mwovu mno. Akiketi kwenye roshani, huko juu katika Indiana ambako tulikuwa tukifanya mkutano, hakuna mtu aliyeonekana kujali. Kama wangalijua alikuwa ni nani, wangalirudi nyuma kutoka kwake.

109 Lakini Yesu alijali. Alinisogeza karibu, na kusema, "Mwanamke anayeketi huko juu, jina lake ni Rosella Griffith. Yeye ni mlevi sugu. Amekatiwa tamaa na Shirika la Walevi, wala hawawezi kumfanyia lolote. Basi matumaini yote yamekwisha. Lakini yeye amemwamini Yeye. BWANA ASEMA HIVI. Tangu saa hii na kuendelea, hakuna pombe tena." Na sasa yeye ni Mkristo mwema, mwenye upendo; mahali mahali, na kutoka baa moja duni hadi nyingine, kutoka jela hadi jela, akiihubiri Injili, kuwaokoa walevi sugu.

110 Yesu hujali, kwa hiyo mtwikeni tu fadhaa zenu. Katika huzuni zenu, Yeye anajali. Ninyi, mnapowapoteza wapendwa wenu, Yeye anajali. Yeye anawajali waliofariki, wale waliokufa katika Kristo.

111 Siku moja, Yeye alikuwa amechoka sana akienda Zake, ilikuwa vigumu Kwake kutembea. Lakini lilikuja ku—kundi la watu kutoka mjini, msafara wa mazishi, naye maskini mama akirusha-rusha mikono yake hewani, na kuiminya. "Ee Yehova, kwa nini ukamchukua? Yeye ndiye mwanangu wa pekee!"

112 Alikuwa amechoka na kudhoofika, lakini alimshughulikia maskini mwanamke huyo mdogo, aliyevunjika moyo. Akaenda kwa wa—wabebaji ambao—ambao walilibeba je—jeneza, naye akaligusa, na kusema, "Mwanangu, amka!" Kwa nini? Yeye alijali.

Yeye anaelewa. Sasa tunajua, kwa maisha Yake, ya kwamba Yeye anajali.

113 Sasa swali ni kwamba, kwa ajili yetu usiku wa leo, je, unajali? Yeye anajali. Lakini sasa wewe unajali? Kama hujali, basi Yeye hawezi kukusaidia. Lakini, kama unajali vya kutosha, ama unajijali vya kutosha! Nimewasikia watu wakitoa tamshi hili la kiwazimu, "Sijali yatakayonipata." Loo, jamani!

Hakika ninajali yatakayonipata. Hakika, najali. Najali. Nami ninaamini mtu yeyote, mwenye akili timamu, hujali. Ninataka kujua yatakayonipata. Na kama ninajua Yeye alinipenda, hakuna mwingine angeweza kupenda jinsi hiyo. Yeye anakujali. Anakujali. Haidhuru wewe ni mdogo jinsi gani, jinsi usivyo na maana, jinsi ulivyo maskini, jinsi usivyojali, ni mara ngapi umejaribu na kushindwa, Yeye angali anajali. Upendo Wake ungali unabisha mlangoni mwa moyo wako. Lakini sisi hatuna shukrani kwa jambo hilo? Katika siku hapa ambapo. . .

114 Ndiyo kwanza niwaambie. Natumaini halikupita juu ya kichwa chako. Natumaini halikupita kwa urahisi, bali mtakumbuka maneno haya. Kwamba, kila kitu kiko mwishoni. Ustaarabu uko kwenye mwisho wake. Demokrasia iko kwenye mwisho wake. Kila kitu! Taifa hili limeoza kwa ndani, wakati wowote litalipuliwa vipande-vipande. Loo! Mataifa mengine, ulimwengu, uko kwenye mwisho wake. Kwa kuwa, kila kitu kipatikanacho na mauti hakina budi kufa, kutopatikana na mauti kupate kupachukua mahali pake. Hatuna budi kupafikia mahali hapa. Tuko hapa. Tuko mwisho. Wala hakuna msingi mwingine, hakuna jambo lingine unaloweza. . .Wala hakuna kitu kingine kinachoweza kujali sasa ila Yesu, Naye kweli anajali.

115 Hivi hujali vya kutosha kuyasalimisha maisha yako Kwake, kumpenda, kwenda mitaani, kumwendea bosi wako, jirani yako, kila mahali, kwa roho tamu, nyenyekevu? Jitengeni na mambo ya ulimwengu, na muishi maisha matulivu sana, matamu, hata wengine watamwona Yesu ndani yenu. Hivi hamjisikii ya kwamba mnamwia hilo? Hebu tusiwe wasio na shukrani, ninyi watu hapa.

116 Jana jioni nilipotoka nje, maskini mwanamke mmoja alikuwa amesimama mlangoni. Natumaini yuko humu usiku wa leo. Nilipopita, alikuwa amesimama pale pamoja na mtoto mchanga. Akaanza kulia. Yeye hakuwa Mkristo. Lakini hakuutaka huo Ujumbe ukatizwe, kwa hiyo akamchukua mtoto wake akatoka nje kisiri pamoja naye. Nilipotoka nje mlangoni, yeye alisema, "Loo, jinsi ningalitaka kusikia mwisho wa huo Ujumbe!" Nami. . .

117 Kitu fulani kikaniambia tu, "Hili si la baha-. . .si la bahati. Hili ni la Mungu."

Nikasema, "Mama, wewe ni Mkristo?"

118 Akasema, "La, bwana. Ninatumaini kuwa siku moja." Maskini mama mwenye sura nzuri, akiwa na mtoto mchanga mkononi mwake.

119 Nikasema, "Yeye yupo hapa. Usiliahirishe muda mrefu kupita kiasi." Na hapo tukaviinamisha vichwa vyetu, pamoja pale, na kuomba. Ndipo nikamwomba Mungu aichukue nafsi yake.

120 Basi mwishowe, nilipomaliza kuomba, akasema, “Amina.” Ndipo akaanza kuyapangusa machozi kutoka machoni mwake.

121 Kwa nini? Alionyesha. Wakati alipoutaka huo Ujumbe, hata hivyo, kama hakuupata, labda alikuwa na mtu mwingine hapa kuupata. Alitaka mtu mwingine aupate.

122 Nalo lilifanya nini? Mungu alijali. Kwa hiyo alimfanya asimame papo hapo, mahali pale pale, apate kuupokea. Jambo ndilo hilo. Yeye anajali. Yeye anajua jinsi ya kuyapanga mambo vizuri. Hivi tuna shukrani vya kutosha?

123 Inanikumbusha juu ya hadithi ya jambo fulani lililotukia katika mji fulani karibu na hapa. Miaka kadhaa iliyopita, mama mmoja alikuwa amemtuma msichana wake kwenda chuoni. Jina lake lilikuwa ni Mary. Na kwa hiyo msichana huyo alikuwa ni msichana mzuri, alipoondoka nyumbani. Alikuwa . . . Mama yake alikuwa akifua kwenye ubao, na kadhalika, apate ku—kumlipia chuo. Basi siku moja alienda kutembea nyumbani. Naye alikuwa amechanganyikana na tabaka la watu waliochangamana. Naye akaingia katika ushirika pamoja na msichana asiyeamini aliyekuwa wa kilimwengu sana na asiye mtauwa.

124 Na ni vibaya unapoanza kushikana na watu kama hao. Jitenge na mambo ya ulimwengu. Toka! Usijaribu kuwa bora zaidi, kujaribu kutenda kana kwamba wewe ni bora zaidi; ila usiyachafue mavazi yako na dhambi. “Usishiriki dhambi za wengine.” Ukitaka kuzungumza neno la kuwatia watu moyo, vema. Lakini haikubidi kugaagaa pamoja na nguruwe! Kaa mbali nao. Hiyo ni kweli.

125 Alikuwa ameshuka kwenye uchafu pamoja na msichana huyo. Ndipo wakati alipokuja nyumbani, garimoshi lilisimama mbele. Ndipo huyo msichana, akiketi kwenye dirisha, aliangalia nje.

126 Basi hapo palikuwako na mwanamke mzee huko nje, ambaye alikuwa na makovu kote usoni mwake, nayo shingo yake imejikunyata, maskini mikono yake ni magofu jinsi hiyo, akiangalia kwa yote yaliyokuwa moyoni mwake, akiangalia mtu fulani ashuke kwenye garimoshi.

127 Basi msichana huyu aliyekuwa pamoja na Mary, akasema, “Mary, hebu angalia maskini mwanamke yule mwenye sura ya kuchukiza!” Kasema, “Hivi yeye si ana sura mbaya sana?” Naye huyo alikuwa ni mama yake Mary.

128 Naye Mary, kwa sababu ya hisia ya rafiki yake, akasema, “Naam, ana sura mbaya. Sana!”

129 Basi walipotoka kwenye garimoshi, Mary ameshikwa kwenye kituo hicho, mama yake alikimbia na kusema, “Loo, kipenzi, nina furaha sana kukuona!”

130 Ndipo Mary akampa mamaye kisogo. Naye akasema, “Sikujui wewe,” na akaanza kuondoka.

131 Basi ikawa mwangalizi alikuwa amesimama pale, naye akaruka kwenye sanduku hili, akasema, “Hebu kidogo!” Naye akauvutia usikivu wa wote waliokuwa karibu. Akasema, “Ewe mtoto wa mateso! Ungewezaje kumpa mama yako kisogo kwa ajili ya maskini msichana huyo asiye na heshima aliye pamoja nawe? Hivi hujionei aibu, Mary?”

132 Kasema, “Nakijua kisa hicho. Sikiliza hapa, ewe msichana,” kwa huyo msichana mwingine aliyekuwa ametoa lile tamshi kulihusu. Kasema, “Huyo ndiye mama yake. Wala Mary kamwe hataiona siku aliyokuwa nusu mrembo kama mama yake. Nilimfahamu wakati alipokuwa mdogo.” Kisha kasema, “Alikuwa ameolewa kwa furaha. Naye akamzaa maskini mtoto huyu mchanga, Mary. Basi alikuwa kwenye orofa ya juu, naye alikuwa ameyafungua madirisha kusudi u—upepo mwanana uninii. . .Nacho maskini kitanda kidogo cha mtoto kule juu.” Naye akasema, “Alishuka chumba cha chini naye alikuwa akifua nguo, akizianika kwenye kitalu cha nyuma. Ndipo moto ukaishika hiyo nyumba. Basi kabla hajatambua hilo, nyumba yote ilikuwa nyekundu kwa moto, majirani wakikimbia. Ndipo mama yake Mary alipokaribia, alisema, yeye alisema, ‘Mtoto wangu! Mtoto wangu, yuko kwenye orofa ya juu!’ Ndipo zimamoto wakasema, ‘Nyumba imeshindikana. Hakuna njia ya kuingia humo sasa.’ Lakini yeye alifanya nini? Alinyakua aproni ndogo kutoka kwake, iliyokuwa imelowa maji ya kufua nguo, akajifunika usoni mwake, na kukimbia kupitia ndimi hizo za moto. Nao polisi wakijaribu kumzuia. Akakimbia kwenye vipandio upesi sana. Kwa nini? Mtoto wake mpendwa alikuwa amelala mle. Ndipo akamnyakua huyo mtoto, naye akawazia, ‘Hili vazi lililolowa maji lilinikinga. Lakini sasa kama nikimrudisha mtoto huyu mchanga, itamkata vipande-vipande, miale hiyo ya moto.’ Hivyo basi akamfunika mtoto huyo mchanga kwa vazi lake mwenyewe lililolowa maji, akamshikilia kifuani mwake, akakimbia kupitia kwenye hiyo miale. Nayo ikazirarua nyama kutoka usoni mwake.”

133 Kasema, “Hiyo ndiyo sababu yeye ana sura mbaya. Ana sura mbaya, ili uweze kuwa mrembo. Nawe wataka kusema ungempa kisogo mama yako aliyejitolea hivyo kwako?” Katika aibu, akainamisha kichwa chake.

134 Nafikiri hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa. Je, Injili hii, Mfariji huyu tuliye naye, Roho Mtakatifu huyu ambaye ulimwengu unamwita “ulokole,” ambao watu wanataka kusema hao ni “watakatifu wanaojibingirisha,” unaona aibu? Unaionea aibu dhabihu ambayo Yesu alitoa kule chini msalabani, ili tuweze kuwa na faraja hii? Ungeweza kuibadilisha kwa faraja ya ulimwengu, umaarufu wa jirani fulani? Mungu aepushe!

135 Na tumtwike fadhaa zetu, kwa maana Yeye anatujali! Na tumpende na kumthamini kwa yote yaliyo ndani yetu!

136 Na, loo, wakati wanafunzi waliporudi, wakifurahi kwa sababu walihesabiwa kuwa wanastahili kubeba shutuma ya Jina Lake, hivyo ndivyo ninavyojisikia usiku wa leo. Sijali, mnaweza kusema mimi "nimerukwa na akili," mnaweza kuniita "mtakatifu anayejibingirisha." Nalo kanisa langu la Kibaptisti liliniambia ningeingia wazimu, ama ningekuwa mtakatifu anayejibingirisha.

137 Baba na mama yangu walinifukuza nyumbani mwao, bila kitu ila mfuko wa karatasi chini ya mkono wangu, pamoja na nguo chache chini yake; shati dogo na nguo za ndani za kubadilisha na jozi chache za soksi, ndizo tu nilizokuwa nazo. Nao watu wangu wenyewe wakasema, "Huwezi kuleta upuuzi huo huku na ubaki mtoto wetu." Ndipo nikaenda New Albany, bila kujua niende wapi, bila mahali pa kukilaza kichwa changu.

138 Lakini, ndugu! Ndipo ibilisi akanijia katika saa hiyo, katika kufa kwa mtoto wangu. Mara nyingi ambapo nimekuja, lakini ninajua ulipo wokovu! Nisingeweza kukanusha Hilo! Ingawa lingeniua, siwezi kulikanusha. Nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa neema ya Mungu. Shida zangu zote ametwikwa Yeye, kwa kuwa Yeye ananijali. Naye anakujali.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu sasa.

139 Na, nashangaa, kama hujawahi kumtwika shida zako zote; huenda ukamtwika baadhi yake, bali kidogo unaogopa tu kumtwika zote. Kama vile mwaminio mkwamia mpakani, kama vile katika Waebrania 10. Ilisema katika Waebrania mlango wa 6, ilisema:

> . . .*kwa kuwa* sisi *tumemsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi* zetu . . .
>
> . . .*na* kuhesabu *damu ya agano* tuliyotakaswa *kwayo kuwa ni kitu ovyo, na . . .kuifanyia jeuri* kazi *za neema*?

140 Waebrania 10, ilisema:

> . . .*kama tukifanya dhambi kusudi baada ya . . . kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi,*
>
> *Bali . . .kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto . . .*
>
> *Maana twajua . . .*
>
> Ni *jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai.*

Wakati kukiwako na rehema, rehema kwenye Chemchemi, nafasi kwenye Chemchemi!

141 Andiko hilo, wakati mkiomba, ningetaka kuwaambia. Maandiko hayo yanarejea kitu gani, "Wakiisha kupewa

nuru, haiwezekani kupata maarifa kamili”? Kama mwaminio mkwamia mpakani, kama vile katika Mwanzo 14, ama wakati—wakati . . . Katika Kutoka, ambapo Waisraeli walikuja kwenye nchi ya ahadi, wakaonja zabibu zenyewe kutoka kwenye nchi ya ahadi; bali wakarudi kwa woga, wamehofu, “Hatuwezi kuvuka, upinzani ni mkuu sana.” Waaminio wakwamia mpakani, watu watakaokuja kanisani, na, loo, waseme, “Ni ajabu,” wala wasiliguse kwa mkono wao. Kamwe hawataki kuanguka chini madhabahuni, na kusema, “Mungu, nijaze na Roho, na jalia niwe mmoja wa watoto Wako.” Wakwamia mpakani! Hatutaki hivyo.

142 Hebu tuwe Mkristo halisi. Hebu kanisa hili lishike moto, mikutano ya maombi ikiendelea wakati wote, mikutano kote mjini, kila mahali; wafanyakazi, haitabidi waambiwe, bali wakifanya kazi kwa hiari wakati wote kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Na kuyaacha makanisa mengine yaliyowakilishwa hapa, jalia wafuasi wake warudi kanisani mwao, wakiwa na ujuzi huo. Tumtwike fadhaa zetu, kwa kuwa Yeye anawajali. Yeye ndiye Mfariji.

143 Endapo kuna mtu kama huyo usiku wa leo, kwa uaminifu ukikiri mbele za Mungu ya kwamba huna hiyo amani, ya kwamba ungeweza kumtwika kila fadhaa, bali unalitaka; umelijaribu, umejikuta kwalo, bali kamwe hujafikia mahali ambapo kweli ungeweza kujitolea kabisa Kwake, nawe ungetaka kufanya hivyo, hivi waweza kusema, “Nikumbuke katika maombi, Ndugu Branham, ninapoinua mkono wangu”? Waweza kuinua mkono wako sasa, useme tu, “Nikumbuke, Ndugu Branham, katika maombi.” Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, dada. Ubarikiwe, na wewe, na wewe hapa. Naam. Na kule nyuma upande wa nyuma, Mungu awabariki. Yeye anaiona mikono yenu ikiinuliwa. Bwana akubariki, mama. Mungu akubariki papa hapa mbele, dada. Na Mungu akubariki huko nyuma, ndugu yangu. Yeye anakujali. Tulizoea kuimba wimbo mdogo:

Anakujali,
Anakujali;
Kupitia mwangaza wa jua ama kivuli,
Anakujali.

144 Mnakumbuka, Arizona, ziara yangu ya kwanza hapa, nanyi mkaniimbia “kwaheri” kwa wimbo huo, maskini kwaya ndogo ya Kihispaniola hapa kutoka kwa kanisa la Ndugu Garcia; wakati tungekusanyika pamoja huko California, wakati niliposhuka mstarini, nikilia, huku tukipungiana mikono. Wengi ni baba na mama, na wengi wao wametuacha wakaingia kwenye pazia huko ng’ambo, usiku wa leo. Lakini Yeye angali anawajali. Yeye ataendelea kujali. Wakati hakuna kitu kingine kinachoweza kujali, Yeye atajali. Mnampenda sasa, nanyi mnataka kuninii . . . Mnataka awashughulikie, nanyi mnataka

kumjali. Inua mkono wako, useme, "Nikumbuke katika maombi, Ndugu Branham. Nina haja usiku wa leo ambayo siwezi kuiweka madhabahuni. Isipokuwa . . . "

145 Nawe uondoke tu, na kumtwika Bwana, na kusema, "Bwana, mimi ni—mimi ni mvuta sigara." Mungu akubariki, ndugu. "Mimi ni mlevi. Mimi ni—mimi ni mwongo. Kamwe siwezi kuacha kufanya mizaha, kufanya mizaha michafu. Kamwe siwezi kuacha kunywa pombe, kinywaji cha umma, ninaingiana na umati. Na—nataka—nataka kuyaondokea hayo yote. Mimi—mimi—mimi ni mtu ambaye daima anatazama vitu viovu, mitaa imejaa wa—wanawake wachafu na wanaume. Na—nami na—nataka—nataka kuachana na hayo. Naomba, Ee Mungu, jalia niweze kuzitwika shida zangu zote, usiku wa leo, Kwako?"

146 Waweza kuinua mkono wako, useme, "Uniombee, Ndugu Branham. Sasa hapa ninasalimisha kila kitu, na kukiweka madhabahuni, nami nitamtwika Yeye shida zangu zote"? Huenda ikawa kuna mwingine kabla hatujaomba?

147 Mungu ambariki huyu, jamaa mdogo anayeketi hapa ameinua mkono wake, jamaa mdogo mwenye fulana nyekundu. "Mtoto mdogo atawaongoza," kweli Maandiko ni ya kweli.

148 Huenda kuna mwingine mahali popote, ungeinua tu mkono wako, na kusema, "Niombee"? Mungu akubariki, mvulana mdogo Mhispaniola anayeketi hapa. Mtu mwingine? Mungu akubariki hapo, mama, ninauona mkono wako. Hapo, bwana, ninauona wako. Na kijana wa Kihispaniola huko nyuma. Na mama huyu anayeketi hapa. Ninaona. Mungu anauona mkono wako, Yeye anajua msisimko wako. Ubarikiwe, dada. Mungu akubariki, ndugu. Hilo ni jema. Mtu mwingine yeyote ambaye angesema, "Unikumbuke, Ndugu Branham"? Mungu akubariki huko nyuma, ewe mwanangu. Mungu akubariki, dada. Na wewe, msichana mdogo unayeketi hapa. Huko nyuma kabisa kule, ninauona mkono wako, mtu huyo mkubwa mwenye nguvu aliyeinua mkono wake hewani. Mungu akubariki unayeketi hapa, jamaa mdogo, katika ubora wa maisha, anayeketi hapa ameinamisha kichwa chake.

149 Loo, ni wakati wa jinsi gani! Maamuzi yanafanywa, "Hivi ninaweza kumtwika fadhaa zangu zote?" Laweza kuonekana la kigeni. Mungu wabariki hawa mtu na mkewe wakongwe kutoka hapa. "Nitamtwika shida zangu." Naam, salimisheni tu kila kitu. Mimi . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] "Hizi hapa shida zangu zote, juu Yako. Ninaamini." Mungu akubariki, huyo msichana huko nyuma, msichana wa Kihispania. Huyo kijana mwanamume. Msichana huyo. Naam. Mungu akubariki. Hilo ni zuri. Huenda kuna mwingine kabla tu ya maombi sasa? Kumbukeni, mnafanya ninii yenu . . .

150 Mbariki mvulana huyu mdogo. Mbariki msichana huyu hapa. Loo! (Nanyi katika maombi, ninataka tu kusema jambo

fulani.) Moja ya mitazamo midogo ya kupendeza sana! Iwapo kuna kesho, yule pale mhudumu ameketi akiniangalia, wa yapata umri wa miaka minne.

151 Sasa kumbukeni, roho ya upambanuzi, sijawa nikiitoa hapa kanisani katika siku moja tu ama mbili zilizopita usiku. Ninataka kupata kitu kingine kwanza. Kunao watu walioketi hapa wakiwa na shuhuda mioyoni mwao (najua hilo), walioponywa miaka kadhaa iliyopita, na mambo haya yote. Lakini nataka kuyatanguliza mambo ya kwanza. Hebu tuzifanye nafsi zetu kusudi tunaweza kumtumainia tu Mungu na kuweka kila kitu madhabahuni, kusema, "Bwana Mungu, mimi hapa."

> Ila kwamba Damu Yako ilimwagwa kwa ajili
>   yangu,
> Na kwamba Wewe waniagiza nije Kwako,
> Ee Mwana-kondoo wa Mungu, naja! Naja!

152 Nashangaa sasa, kwa kuwa wengi wameinua mikono yao . . .

153 Kuna kitu fulani kuhusu kanisa, ambacho ni kitamu. Ni mahali ambapo watakatifu wanakutanika pamoja, wakati baada ya wakati, kuomba, ambapo huduma inahubiriwa jukwaani. Kuna kitu fulani cha kupendeza kuhusu kanisa. Ulimwengu umejaa watu sana siku hizi, kidogo ni vigumu kufanya uamsho ndani ya kanisa, watu wanasimama, wamesongamana.

154 Na ndugu yangu na dada wa thamani, yapata miaka kumi na miwili iliyopita niliwajia, kama kijana mwanamume nikianza huduma. Wengi wenu mngali hapa. Ninamwona Bibi Waldrop hapa. Ambapo, alibebwa akaingizwa mle, amekufa, kwenye machela, akiwa na kansa moyoni; hiyo imekuwa miaka kadha iliyopita. Naye Roho Mtakatifu akamfufua tena. Madaktari wake walitoa ushuhuda wao nao walikuwa na kumbukumbu zake. Wengine wameketi hapa ambao . . . Imethibitishwa, enyi marafiki, ya kwamba Yeye anawapenda.

155 Mwaweza kupanda huku usiku wa leo sasa? Nyinyi mlioinua mikono yenu, mlio na kitu mnachotaka kumtwika Bwana, mnajali, mwaweza kuja hapa na kuniacha tu niwaombee? Njoni, simameni. Ninyi msiomjua Kristo kama Mwokozi wenu. Ama endapo mnamjua, nanyi mna tabia ambazo hamwezi kuziondoa, ama kitu fulani, mwaweza kuja hapa? Msione aibu sasa. Sema, "Niliinua mkono wangu, Ndugu Branham." Basi hakika ungekuja hapa na kusema, "Ninakiri hadharani ya kwamba ninamhitaji Kristo. Ninataka kuja hapa na kusimama."

156 Yeye alisema, "Ukinionea haya, mbele za watu, nitakuonea haya, mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu. Lakini kama utanikiri mbele za watu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu."

157 Mnaweza kutembea na kuja moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa sasa? Njoni moja kwa moja hapa na kusimama.

158 Msichana anakuja, labda ama. . .Nadhani ni mwanamke wa Kichina, akishuka kuja sasa kufanya maungamo yake ya hadharani ya kwamba anamhitaji Kristo. Mungu akubariki, dada. Papo hapo. Nitakuwa pamoja nawe katika dakika moja.

159 Wengine zaidi wanaweza kuja sasa hivi wakati tukiimba? Mungu akubariki, bwana.

Kwa upole na utamu. . .

160 Sasa kama unataka kumtwika fadhaa zako, njoo, jirushe mwenyewe kwenye madhabahu Yake hapa.

Anakuita wewe. . .

161 Simama tu moja kwa moja, uje hapa chini. Tunataka kusimama hapa na kuomba pamoja nanyi, tuwawekee mikono.

Angalia kwenye yale malango Yeye anangojea
na kuangalia,
Akiangalia. . .

162 Anaangalia nini? Anaangalia aone kama kweli ulimaanisha hilo, ama la. Njoni sasa, njoni. Mlimaanisha hilo? Hakika, mlimaanisha.

Njoni nyumbani. . .?. . .njoni. . .

Mungu akubariki. Mungu akubariki, kijana mwanamume hapo.

Ninyi mliochoka, njoni nyumbani;
Kwa bidii, (Mungu!) kwa upole, Yesu. . .

163 Je, una shida usiku wa leo usiyoweza kuiondoa, unataka kumtwika Bwana? Shuka uje.

. . .Loo, mwenye dhambi, njoo nyumbani!

Njoni nyumbani, njoni nyumbani,
Ninyi mliochoka, njoni nyumbani;

164 [Ndugu Branham anaondoka mimbarani na kuomba pamoja na watu madhabahuni, maneno yako hayatambulikani. Ndugu mmoja anaongoza uimbaji na kuzungumza na kusanyiko—Mh.]. . .?. . .

Ingawa tunayo. . .

165 Hivi huwezi kuja sasa, moja kwa moja huku, ukapige magoti, kwa ajili ya maombi. Ninyi ambao hamjaridhika, mahali tu mnaposimama, hivi hamtakuja? Njoni.

. . .kwa ajili yako na yangu.

Njoo nyumbani,

Mungu akubariki, kijana mwanamume. Mungu akubariki, ndugu.

. . .nyumbani,
Ninyi mliochoka, njoni nyumbani;

166 [Ndugu Branham tena anaondoka mimbarani na kuomba pamoja na watu madhabahuni, maneno yake hayatambulikani. Ndugu mmoja anaongoza uimbaji na kuzungumza na kusanyiko—Mh.] . . .?. . .

Njoo nyumbani . . .

167 Je, kunaye yeyote hapa asiye na Roho Mtakatifu, ambaye hajapata kujazwa na Roho wa Mungu, nawe huna hakika na msimamo wako? Inua mkono wako, useme, "Sijampokea Roho Mtakatifu, Ndugu Branham." Mumempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini? Kama hamjampokea, inueni mikono yenu. Mngetaka kuja na kupiga magoti papa hapa sasa, na kuacha tuwaombee, mkampokee Roho Mtakatifu? Njoni sasa wakati tukiimba.

Njoni nyumbani, njoni nyumbani,
Ninyi mliochoka, njoni nyumbani;
Kwa bidii, kwa upole, Yesu anaita,
Anaita, Ee mwenye dhambi, njoo nyumbani!

Kwa nini tungoje wakati Yesu . . .

168 Hivi huwezi kuja sasa, moja kwa moja huku, sasa wakati Yesu anaita? Huenda ikawa ndio wito wako wa mwisho. Hatujui. Huenda usiwe; bali hata hivyo waweza kuwa. Hivi hutakuja? Usibahatishe juu ya hilo. Kama huna hakika, njoo sasa. Je, utakuja?

. . . kukawia wala usikubali rehema Zake,
Rehema kwa ajili yako na yangu?

Njoo nyumbani . . .

Mungu akubariki, ndugu, dada.

. . . nyumbani,
Ninyi mliochoka . . .

169 Itakubidi kuuchukua kutoka hapa, ndugu. Mungu akubariki.

60-0301 Anakujali
First Assembly Of God
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org